

Vitendawili vya kiswahili na majibu yake

A

1. Adui lakini po pote uendako yuko nawe. Inzi
2. Afahamu kuchora lakini hajui achoracho. Konokono
3. Afuma hana mshale. Nungunungu
4. Ajenga ingawa hana mikono. Ndege
5. Ajifungua na kujifunika. Mwavuli
6. Akitokea watu wote humwona. Jua
7. Akitokea watu wote hunungunika na kuwa na huzuni. Ugonjwa
8. Akivaa nguo hapendezi, akiwa uchi apendeza. Mgomba
9. Alipita mtu ana bunda la mshale. Mkindu
10. Alipita mtu mwenye kibandiko cha nguo. Inzi
11. Aliwa, yuala; ala, aliwa. Papa
12. Amchukuapo hamrudishi. Kaburi
13. Amefunika kote kwa blanketi lake jeusi. Giza
14. Amefunua jicho jekundu. Jua
15. Ameingia shimoni akiwa uchi, akatoka amevaa nguo nzuri. Mbegu
16. Amejitwika mzigo mkubwa kuliko yeye mwenyewe. Konokono/Koa
17. Amekaa kimya na watoto wamemzunguka pande zote. Mgomba
18. Amekula ncha mbili. Wali
19. Amevaa joho kubwa kuliko yeye mwenyewe. Kaburi
20. Anakuangalia tu wala halali au kutembea. Picha
21. Anakula kila siku lakini hashibi na hatashiba. Mchanga

22. Anakula lakini hajashiba na hatashiba milele. Ardhi
23. Anakula lakini hashibi. Mauti
24. Anapendwa sana ingawaje ni mkali sana. Moto
25. Anatoka kutembea, anakuja nyumbani anamwambia mama, 'Nieleke'. Kitanda
26. Ashona mikeka wala hailali. Maboga
27. Askari wangu wote wamevaa kofia upande. Majani
28. Askari wangu wote wamevaa mavazi meusi. Chunguchungu
29. Asubuhi atembea kwa miguu mine, adhuhuri kwa miwili. Fedha
30. Atapanya mbegu nyingi sana lakini hazioti. Mvua
31. Atolewapo nje hufa. Samaki

B

32. Baba alinipa mfupa, nikautunza ukawa fahali. Muwa
33. Baba ameweka mkuki nje nikashindwa kuukwea, mdogo wangu akaukwea. Sisimizi
34. Babako akojoapo hunung'unika. Mawingu
35. Babu amefunga ushanga shingoni. Mtama/Nazi
36. Babu anakula ng'ombe, analea fupa linakuwa ng'ombe. Muwa
37. Babu hupiga kelele akojoapo. Mvua
38. Babu mkubwa ameangushwa na babu mdogo. Mti na shoka
39. Babu, nyanya, mjomba, mama, baba na watoto, mna safari ya wapi? Siafu
40. Bak bandika, bak bandua. Nyayo
41. Bawabu mmoja tu asiyeogopa chochote duniani. Mlango
42. Bibi kikongwe apepesa ufuta. Kope za macho
43. Bibi yake hutandikwa kila siku, lakini hatoroMoyoKinu cha kutwangia

C

44. Chakula kikuu cha mtoto. Usingizi
45. Cha ndani hakitoki nje, cha nje hakiingii ndani. Nyama na mfupa
46. Chang'aa chapendeza, lakini hakifikiwi. Jua
47. Chatembea na hakijapata kupumzika hata nukta moja. Mwezi/Jua
48. Cheupe chavunjika manjano yatokea. Yai
49. Chumba change kina ukuta niondoa na kuusimika nitakapo. Pazia
50. Chungu change cha udongo hakipasuki kikianguka. Mjusi/Panya
51. Chungu kikubwa sana chenye kifuniko kikubwa sana. Dunia na mbingu

D

52. Dada yangu akitoka kwao harudi kamwe. Jani likwanyukapo
53. Dada yangu kaoga nusu. Jiwe mtoni
54. Drrrrrh1 Ng'ambo. Daraja la buibui
55. Dume wangu amelilia machungani. Radi

F

56. Fahali wa ng'ombe na mbuzi wadogo machungani. Mwezi na nyota angani
57. Fika umwone umpendaye. Kioo
58. Fuko kajifukia, mkia kaacha nje. Kata mtungini
59. Funga mizigo twende Kongo. Mikia ya mbwa

H

60. Hachelewi wala hakosei safari zake. Jua
61. Haina miguu wala mikono, lakini, yabeba magogo. Maji
62. Hakihitaji maji, wala udongo, wala chakula; lakini chamea. Nywele
63. Hakionekani wala hakishikiki. Hewa
64. Hakisimami, na kikisimama msiba. Moyo

65. Hakuchi wala hakuchwi. Kula
66. Halemewi wala hachoki kubeba. Ardhi
67. Hamwogopi mtu yeyote. Njaa
68. Hana mizizi, nimemkata mara nyingi lakini haachi kukua. Ukucha
69. Haoni kinyaa. Mvua
70. Hapo nje panapita mtu mwenye miguu mirefu. Mvua
71. Hasemi, na akisema hatasahaulika. Kalamu
72. Hasimamishwi akiwa na ghadhabu. Upepo
73. Hata inyeshe namna gani haifiki humu. Kwapani
74. Hata jua likiwaka namna gani hakauki wala kupata joto. Pua ya mbwa
75. Hata Mzungu ameshindwa. Mauti
76. Hauchagui chifu wala jumbe. Utelezi
77. Hausimiki hausimami. Mkufu
78. Hawa wanaingia hawa wanatoka. Nyuki mzingani
79. Hesabu haihesabiki. Nyota
80. Huitumia kila siku lakini haiishi. Miguu
81. Huku kutamu, huku kutamu, katikati uchungu. Jua
82. Huku unasikia 'pa' Huku unasikia 'pa! Mkia wa kondoo
83. Hula lakini hashibi. Sindano
84. Hulala tulalapo, huamka tuamkapo. Jua
85. Humu mwetu tuko wanne tu, ukimwona wa tano mwue. Matendegu ya kitanda
86. Huna macho lakini wakamata wanyama. Ndoana
87. Hupanda mtini na mwenye kichaa wake. Kivuli
88. Hutembea watatu. Mafiga

89. Hutoka upesi sana lakini hasalimu. Kuku

90. Huwafanya watu wote walie. Moshi

91. Huwezi kukalia alipokalia msichana wangu mweusi. Chungu jikoni

92. Huzikwa mmoja, hufufuka mmoja, huzeeka wengi. Mbegu na matunda

I

93. Inaonekana mara mbili katika dakika moja na mara moja tu katika mwaka. Herufi "K"

94. Ini la ng'ombe huliwa hata na walioko mbali. Kifo

J

95. Jembe la Wangoni haliishi. Miguu/Nyayo

96. Je, unaweza, kukua ukampita mzee wako? Nywele kichwani

97. Jiwe litoalo maji. Macho

K

98. Kaburi la mfalme lina milango miwili. Kata ya kuchukulia Maji kichwani

99. Kaka yangu anapanda darini na fimbo nyuma. Paka na mkia wake

100. Kama kingekuwa mkuki, ungekuta kimekwisha kuua wote. Kizingiti cha mlango

101. Kama unapenda, mbona usile? Ulimi

102. Kanipa ngozi nikapikia, kanipa nyama nikala, kanipa mchuzi nikanywa, kanipa mfupa nikautumia. Nazi

103. Kapanda mti pamoja na uchawi wake. Tumbaku inaponuswa puani

104. Kidimbwi kimezungukwa na majani. Macho

105. Kikioza hutumiwa, kikiwa kichungu hakitumiwa. Maziwa

106. Kila linapofika kwetu hutanguliza makelele. Mvua

107. Kila mtu atapitia malango huo. Kifo

108. Kila mtu hata mfalme huheshimu akipita. Mlango

109. Kila siku hupita njia hiyo hiyo bali arudipo hatumwoni. Jua
110. Kileee! Hiki hapa. Kivuli
111. Kilimsimamisha chifu njiani. Chawa
112. Kina mikono na uso lakini hakina uhai. Saa
113. Kinaniita lakini sikioni. Mwangwi
114. Kisima cha Bimpai kina nyoka muwai, ndiye fisadi wa maji. Taa ya utambi
115. Kisima kidogo kimejaa changarawe. Kinywa na meno
116. Kitendawili change ukikitambua nitakupa hirizi. Mimba
117. Kiti cha dhahabu hakikaliwi na watu. Moto
118. Kiti cha Sulatni hukaliwa na mwenyewe. Kuku aatamiapo mayai
119. Kiti nyikani. Uyoga
120. Kitu changu asubuhi chatembea kwa miguu mine, saa sita kwa miguu miwili, jioni kwa miguu mitatu. Maisha ya binadamu
121. Kiwanja kizuri lakini hakifai kuweka mguu. Kipara
122. Kombe ya Sultani li wazi. Kisima
123. Kondoo wangu amezaa kwa paja. Mhindi
124. Kondoo wangu mnene kachafua njia nzima. Konokono
125. Kondoo za mtoto zamaliza mavuno. Jiwe la kusagia
126. Kufanya kwa ridhaa mojamoja. Kusuka mkeka
127. Kuku wangu aliangua mayai jana, lakini si kuku wala ndege. Nyoka au samaki
128. Kuku wangu amezalia miibani. Nanasi au chungwa
129. Kuku wetu hutagia mayai mikiani. Matunda
130. Kuna mlima mmoja usio pandika. Nafasi kati mdomo na pua
131. Kuna mtu mwenye tumbo kubwa aliyesimama nje. Ghala

132. Kuna ziwa kubwa ambalo limekauka na limebakiza mizizi. Chongo

133. Kunguru akilia hulilia mirambo. Mtoto akililia maziwa

134. Kwenye msitu mkubwa Napata mti mmoja tu, lakini kwenye msitu mdogo naweza kupata miwili. Watoto wa ng'ombe na mbuzi

135. Kwetu mishale na kwenu mishale. Mikia ya panya

136. Kwetu twalala tumesimama. Nguzo za nyumba

L

137. La mgambo limelia wakatoka weusi tu. Chunguchungu

138. Likienda hulia, likirudi halilii. Debe aka buyu

139. Likitoka halirudi. Neno

140. Liwali amekonda lakini hana mgaga. Sindano

M

141. Mama ametengeneza chakula lakini hakula. Chungu cha kupikia

142. Mbona kinakumeza lakini hakikuli? Nyumba

143. Mbona mwakunjiana ngumi bila kupigana? Mafiga

144. Mbona mwasimama na mikuki, mwapigana na nani? Katani

145. Mchana 'ti' usiku 'ti'. Mlango

146. Mdogo lakini humaliza gogo. Mchwa

147. Mfalme amesimika mkuki wake hapa name nikausimika wangu kando yake, baadaye hatukuitambulisha tena. Kohozi

148. Mfalme hushuka kwa kelele. Mvua

149. Mfalme katikati lakini watumishi pembeni. Moto na mafiga

150. Mfalme wetu hupendwa sana, lakini wakati wa kumwona lazima umtoe nguo zote kwanza.

Hindi

151. Mhuni wa ulimwengu. Inzi
152. Mkanda mrefu wafka mpaka pwani. Njia
153. Mke wangu mfupi, lakini huvaa nguo nyingi. Hindi
154. Mlango wa nyumba yangu uko juu. Shimo la mchwa
155. Mlima mkubwa wapandwa kuanzia juu. Sima/Ugali
156. Mlimani sipandi. Maji
157. Mlima umezuia kutazama kwa mjomba. Kisogo
158. Mlima wa kupanda kwa mikono. Mlima
159. Mlima wa kwetu hupandwa na mfalme. Nafasi kati ya mdomo na pua ya ngombe
160. Mlima wa mwenyewe hupandwa na mwenyewe. Buibui na utando wake
161. Mpini mmoja tu lakini majembe hayahesabiki. Mkungu wa ndizi
162. Msitu ambao haulii hondohondo. Mimba
163. Mti mkubwa, lakini una matawi mawili tu. Kichwa na masikio
164. Mti mnyanya mti kerekeche mti ah mti ah!. Ngoma na upatu
165. Mti wangu una matawi kumi na mawili na kila tawi lina majani kadiri ya thelathini. Mwaka
166. Mtoto asemea pangoni. Ulimi mdomoni
167. Mtu mdogo mwenye miguu mirefu ambaye aweza kutembea dunia nzima kwa dakika tano. Mawazo
168. Mvua hema na jua hema. Kobe
169. Mvua kidogo ng'ombe kaoga kichwa. Jiwe
170. Mwadhani naenda lakini siendi. Jua
171. Mwalimu analala na mwanafunzi wanamsomea. Kinyesi na inzi
172. Mwanamke mfupi hupiga kelele njiani. Kunguru
173. Mwanamke mfupi hutengeneza pombe nzuri. Nyuki

174. Mwanang'ang'a hulia mwituni. Shoka
 175. Mwepesi, lakini aweza kuvunja nyumba za mji wote. Tufani
 176. Mwezi wangu umepasuka. Kweme
 177. Mzee Kombe akitoa machozi wote hufurahi. Mvua
 178. Mzee Kombe akilia watu hufurahi. Mvua
 179. Mzizi wa miti hutokea mbali. Siafu
 180. Mzungu yuko ndani na ndevu ziko nje. Hindi
- N
181. Naitumia ngazi hiyo kwa kupandia na kushukia. Mwiba
 182. Nakikimbilia lakini sikikuti. Njia
 183. Nakupa lakini mbona huachi kudai. Tumbo
 184. Nakwenda msituni na mdogo wangu, lakini yeye namwacha huko.
 185. Nameza lakini sishibi. Mate
 186. Namkimbiza lakini simkuti. Kivuli
 187. Namlalia lakini hali. Kitanda
 188. Namwomba atangulie lakini hukataa kabisa. Kigino
 189. Nanywa supu na nyama naitupa. Muwa
 190. Napigwa na mvua na nyumba ipo. Matunda ya pua/Kwapa
 191. Natembea juu ya miiba lakini hainichomi. Miiba
 192. Natembea juu ya miiba lakini sichomwi. Ulimi
 193. Natembea na wenzangu lakini tukifika kwenye nyumba mimi hukaa mlangoni. Mbwa
 194. Natengeneza mafuta lakini nimepauka sana. Mzinga was nyuki kwa nje
 195. Natengeneza mbono lakini alama hazionekani. Mzinga wa nyuki
 196. Ndege wengi baharini. Nyota

197. Ndugu wawili wafanana sana, lakini hawatembeleani. Macho
198. Ngoja nikumbuke. Boga changa
199. Ng'ombe wa baba watelemka mtoni. Mawe mtoni
200. Ng'ombe wa babu huchezea miambani. Mijusi
201. Ng'ombe za babu zikienda machungani hulia, zikirudi hazilii. Vbuyu
202. Ng'ombe za babu zinalala na mkia nje. Viazvi vitamu udongoni
203. Ng'ombe wamechanganyika nikakosa wa kwangu. Pesa/Nyayo
204. Ng'ombe wangu ni weupe kwatoni. Katani
205. Ng'ombe wangu wote hunywa maji isipokuwa mmoja. Fimbo ya kuchunga
206. Ngozi ndani nyama juu. Firigisi
207. Nguo ivaliwayo kila siku isiyoingiwa na chawa. Nyusi
208. Nikicheka kinacheka, nikinuna kinanuna. Kioo
209. Nikienda arudi, nikirudi aenda. Kivuli majini
210. Niiita 'baba' huitika 'baba'. Mwangwi
211. Nikija kwenye ndege wananifukuza, na nikienda kwenye wanyama hawanitaki. Popo
212. Nikimpiga huyu huyu alia. Utomvu wa papai
213. Nikimpiga mambusu. Puliza kidole wakati unapojikwaa
214. Nikimwita hunijibu nani. Mwangwi
215. Nikipewa chakula nala bali natema. Shoka
216. Nikitembea walio wafu huniamkia na walio hai hukaa kimya. Majani makavu na mabichi
217. Nikitembea yuko, nikikimbia yuko, nikiingia ndani hayupo. Kivuli
218. Ni kitu gani ambacho kutoa ni kuongeza? Shimo
219. Nikitupa mshale wangu mchana huenda mbali sana, lakini niutupapo usiku hauendi mbali.

Jicho

220. Nikiwaambia ondokeni hukataa, lakini mjomba akitokea wote hukimbia. Umande na jua

221. Nilijenga nyumba yangu nikaiacha bila kuiezeka majani; lakini niliporudi nilikuta imekwisha ezekwa majani. Mahindi machanga

222. Nilijenga nyumba yangu yenye mlango mmoja. Jani la mgomba la nchani

223. Nilimkata alafu nikamridhia. Kupanda mbegu

224. Nilimtuma askari vitani akaniletea kondoo mweusi. Fuko

225. Nilipandia majanini nikashukia majanini. Mwiba

226. Nilipigwa na tonge la ugali la moto nilipopita msituni. Manyigu

227. Nilipitisha mkono wangu chini la ardhi, nikamshika beberu mkubwa sana. Kiazi kikuu

228. Nilipoangalia kwenye magereza ya Wazungu, nikaona wameketi juu ya mabati. Pelele

229. Nilipofika msituni nilikuta chungu cha pure kinachemka. Mzinga wa nyuki

230. Nilipoingia Rumi, alitoka mtu na wake kumi; kila mke na tundu kumi, kila tundu na kuku kumi; kila kuku na mayai kumi. Mayai, kuku, tundu, wake, kumi kumi kumi. Wangapi walikwenda Rumi? Hakuna

231. Nilipo, juu kuna miiba na chini vivyo hivyo; lakini sichomwi. Ulimi kinywani

232. Nilipokuwa mchanga nilikuwa na kijikia lakini sasa sinacho. Chura

233. Nilitembea na mwezangu naye hupita vichakani. Kivuli

234. Nimechoma fimbo yangu pakabaki pa kushikia tu. Njia

235. Nimefyeka mitende yote kiungani isipokuwa minazi miwili tu. Masikio

236. Nimejenga nyumba babu akaihamia kabla mimi sijahamia. Mjusi

237. Nimekata mti, akaja samba mwekundu akaukalia. Utomvu

238. Nimekata mti bara ukaangusha matawi pwani. Nzige

239. Nimekwenda na rafiki yangu kwa jirani, yeye akafika kabla yangu. Sauti ya nziga

240. Nime tahiri binti wangu akatoa damu mchana kutwa. Kivuli

241. Nimempeleka kondoo wangu akatoa damu mchana kutwa. Mgomba
242. Nimemtuma mtu kumwamkua mtu, yeye amekuja, Yule aliyetumwa hajaja. Kuangua tunda
Ana nazi
243. Nimemwacha mzee kikongwe mtoni anangojea mgeni kulaki. Mtego
244. Nimempandikiza mti wangu ukapeleka matawi ng'ambo ya mto. Kivuli
245. Nimesimama mbali nyikani lakini naonekani. Moto
246. Nimetembea kitambo, kukumbuka sikufunga nyumba. Dirisha Ana ufa
247. Nimetoka kutembea kutembea, nikashika ng'ombe mkia. Kata
248. Nimetupa mshale angani wala sitambui utateremsha ndege wa namna gani. Mimba
249. Nimeweka ndizi yangu, asubuhi siioni. Nyota
250. Nimezaliwa na mguu mmoja. Uyoga
251. Nimezungukwa na adui wengi, lakini siumizwi. Ulimi na meno
252. Nina kijiti change, nizidivyo kukikata ndivyo kizidivyo kuwa kirefu. Maisha
253. Nina kitu changu kitumiwacho na wengine kuliko mimi. Jina
254. Nina kitu kizuri sana nyumbani, lakini siwezi kukichukua. Dada
255. Nina kitu nipendacho ambacho hata baba, mama, dada, kaka hata na mgeni nimpendaye
sana siwezi kumwazima. Mke
256. Nina mwezi ndani ya bakuli. Maziwa
257. Nina ng'ombe wangu nisipomshika mkia hali majani. Jembe
258. Nina nyumba yangu imezungukwa na mifupa. Mdomo
259. Nina pango langu lilojaa mawe. Kinywa
260. Nina watoto wangu hamsini na wote nimewavisha visibau vyeupe. Kunguru
261. Nina watoto watatu, mmoja akitoka kazi haifanyiki. Mafiga
262. Nina badilika umbo langu baada ya kila muda mfupi. Kivuli

263. Ninachimba mizizi ya mti usio na mizizi. Jiwe
264. Ninacho, nakitumia, lakini kila nikitumiapo, sikiharibu ila nakipa rangi. Maji na mkojo
265. Ninakula vitu vyote vinono lakini sikui wala sinenepi. Chungu cha kupikia
266. Ninakwenda naye na kurudi naye. Kivuli
267. Ninao mlima ambao una msitu kileleleni tu. Kichwa
268. Nitokeapo kila mmoja asema namtazama yeye tu. Jua au mwezi
269. Njia yapitwa siku zote lakini haina alama. Njia ya jua au mwezi
270. Njoo hapa nije hapo. Kiraka
271. Nne nne mpaka pwani. Matendegu
272. Nusu mfu nusu hai. Sungura alalapo
273. Nyama ndogo imewashibisha wengi wala isiishe. Kinoo
274. Nyama ya Reale haijai kikombe. Mkufu
275. Nyanya yako ana huruma kukubeba ulalapo. Kitanda
276. Nyumba yangu ina makuti tele, lakini mvua ikinyesha huvuja. Mwembe
277. Nyumba yangu ina milango mingi. Kichuguu
278. Nyumba yangu ina nguzo moja. Uyoga
279. Nyumba yangu kubwa, haina mlango. Yai
280. Nyumba yangu kubwa, haina taa. Kaburi
281. Nyumba yangu kubwa hutembelewa mgongoni. Konokono
- O
282. Oh! Mwanamke aliyevunja chungu mshangao wake
283. Ondoka nikae. Maji ya mfereji
- P
284. Paa alipenga hata pua ikapasuka. Mbarika

285. Palikuwepo watu watatu wakivuka mto. Mmoja alivuka pasipo kukanyaga maji wala kuyaona; wa pili aliyaona maji lakini alivuka bila kuyakanyaga; wa tatu aliyaona na kuyakanyaga alipovuka.

Ni nani hawa? Was kwanza in Mtoto tumboni mwa mamake, was pili ni Mtoto aliyebebwa mgongoni, was tatu ni mama mwenyewe

286. Panda ngazi polepole. Sima ya ugali

287. Para hata Maka. Utelezi

288. Pete ya mfalme ina tundu katikati. Kata ya kuchukulia mizigo

289. Poopoo mbili zavuka mto. Macho

290. Po pote niendako anifuata. Kivuli

R

291. Rafiki yangu ana mguu mmoja. Uyoga

292. Reli yangu hutandika ardhini. Siafu

293. Ruka Riba. Maiti

S

294. Shamba langu kubwa lakini mavuno hayajazi kiganja. Nywele kichwani

295. Shamba langu miti mitano tu. Mkono wa vidole

296. Shangazi yangu ni mrefu sana lakini hafikii tumbo la kondoo. Njia

297. Sijui aendako wala atokako. Upepo

298. Sijui afanyavyo. Nyoka apandavyo mtini

299. Sina dada wala kaka, lakini baba wa huyu jamaa ni mtoto wa babangu. Ni nani huyo?

Mtoto wangu

300. Subiri kidogo! Miiba

301. Sultani alipiga mbiu watu waje kufanya kazi yake lakini wakashindwa. Maji

T

302. Taa ya bure. Jua au mwezi
303. Taa ya Mwarabu inapepea. Kilemba
304. Tajiri aniweka mfukoni na maskini anitupa. Makamasi
305. Tandika kitanga tule kunazi. Nyota
306. Tangu kuzaliwa kwake sijamwona asimame wala kukimbia. Mkufu
307. Tatarata mpaka ng'ambo ya mto. Utando wa baibui
308. Tatu tatu mpaka pwani. Mafiga
309. Tega nikutegue. Mwiba
310. Teke teke huzaa gumugumu, na gumugumu huzaa teke teke. Mahindi ama yai
311. Tengeneza kiwanja kikubwa kabila Fulani lije kupigania. Mbono
312. Tonge la ugali lanifikisha pwani. Jicho
313. Tukate kwa visu ambacho hakitakatika. Maji
314. Tulikaribishwa mahali na mdogo wangu, yeye akaanza kushiba kabla yangu. Kucha
315. Tuliua ng'ombe na babu, kila ajaye hukata. Kinoo
316. Tuliua ng'ombe wawili ngozi ni sawasawa. Mbingu na nchi
317. Tumvike mwanamke huyu nguo. Kuezeka nyumba
318. Tunajengajenga matiti juu. Mapapai
319. Twamsikia lakini hatumwoni. Sauti

U

320. Ukimcheka atakucheka, ukimwomba atakuomba. Mwangwi
321. Ukimwita kwa nguvu hasikii, lakini ukimwita polepole husikia. Fisi
322. Ukimwona anakuona. Jua
323. Ukitaka kufahamu ana mbio, mwonyeshe moto. Kinyonga

324. Ukitembea ulimwengu wote utakosa nyayo. Mwamba
325. Ukiukata haukatiki, ukiushika haushikiki. Moshi
326. Ukiwa mbali waweza kumwona Fulani umatini. Tundu LA sindano
327. Ukoo wa liwali hauna haya. Wanyama
328. Ule usile mamoja. Kifo
329. Umempiga sungura akatoa unga. Funds LA mbuyu
330. Unatembea naye wote umjiao atakuona. Bakora
331. Upande wote umjiao atakuona. Kinyonga
332. Ushuru wa njia wKujikwaa Kujikwaa
333. Utahesabu mchana na usiku na hutamaliza kuhesabu. Nywele
- V
334. Viti kumi nyumbani, tisa vyakalika lakini kimoja hakikaliki. Moto
- W
335. Wake wa mjomba kimo kimoja. Vipande vya kweme
336. Wako karibu lakini hawasalimiani. Nyumba ama kuta zinazoelekeana
337. Wanakuja mmoja mmoja na kujiunga kuwa kitu kimoja. Matone ya mvua
338. Wanameza watu jua linapokuchwa. Nyumba
339. Wanamwua nyoka. Watu wanaotwanga
340. Wanangu wawili hugombana mchana, usiku hupatana. Mlango
341. Wanao wakati wao wa kuringa, nao ni weupe kama barafu. Nyota
342. Wanapanda mlima kwa makoti mazuri meusi na meupe. Vipepeo
343. Wanastarehe darini. Panya
344. Wanatembea lakini hawatembelewi. Macho
345. Watoto wa mtu mmoja hulala chini kila mwaka. Maboga

346. Watoto wangu wana vilemba, asio kilemba si mwanangu. Fuu

347. Watoto wangu wote nimewavika kofia nyekundu. Jogoo

348. Watoto wangu wote wamebeba vifurushi. Vitovu

349. Watu ishirini walipanda juu ya mti, wawili wakaona chungwa, watano wakalichuma, kumi wakalimenya, wote wakaridhirika mtu mmoja alile. Je, ni watu gani hao? Waliopanda ni vidole vya miguu na mikono, walioona ni macho mawili, waliochuma ni vidole vitano vya mikono, waliomenya ni vidole vya mikono yote miwili, na aliyelila ni mdomo

350. Watu waliokaa na kuvaa kofia nyekundu. Kuku, katani au mahindi

351. Watu wamehama askari wekundu wakazidi nyikani. Viroboto

352. Watu wawili hupendana sana; kati ya mchana hufuatana ingawa mmoja ni dhaifu. Usiku mdhaifu

haonekani tena. Kivuli

353. Watu wote ketini tumfinye mchawi. Kula ugali

354. Wewe kipofu unaenda wapi huko juu? Mkweme

Y

355. Yaenda mbali lakini haiondoki ilipo. Njia

Z

356. Zilitazamana na mpaka sasa hazijakutana. Kingo za mto

357. Ziwa dogo linarusha mchanga. Chungu jikoni

358. Ziwa kubwa, lakini naogelea ukingoni tu. Moto